



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA



Simu Na. 028-2520061
Nukushi Na. 028-2520061
Barua pepe: info@geitadc.go.tz
Tovuti: www.geitadc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
S.L.P 139,
GEITA.

07/11/2023.

TAARIFA KWA UMMA

**KUCHUKUA TAHADHARI KUTOKANA NA MVUA ZINAZOENDELEA KUNYESHA
WILAYANI GEITA**

Halmashauri ya Wilaya ya Geita chini ya Mkurugenzi wake ndugu Karia Rajabu Magaro inapenda kuwakumbusha na kuwasisitiza wananchi wa maeneo yote kuendelea kuchukua tahadhari kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani Geita.

Pia watendaji wa vijiji vyote kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kuchukua tahadhari katika maeneo yao, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa Kamati ya Maafa kwa madhara yanayojitokeza kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Aidha Wananchi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za utabiri kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ikiwa ni pamoja na kuzingatia tahadhari zinazotolewa kila siku kutoka kwa wataalam ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini Tanzania (TMA) imesema matukio ya vifo, magonjwa ya mlipuko na uharibifu wa miundombinu yatashuhudiwa kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba 2023 kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha zikichangiwa na El-Nino.

Hendrick K. Msangi

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**